

**GRADE 2 END TERM 3 MARCH 2022**  
**KISWAHILI**

JINA .....

Nambari ya mwanafunzi    Jinsia: Mvulana  Msichana

Jina la shule ..... Msimbo wa shule

Mwalimu ajaze jedwali hili baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi

Sehemu ya	Alama	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
1 Kusikiliza na kuzungumza					
2 Kusoma					
3 Sarufi					
4 Kuandika					

**SEHEMU YA 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA**

1. Dereva ni mtu ambaye huendesha nini?
2. Baiskeli huwa na magurudumu mangapi?
3. Eropleni husafiri wapi?
4. Taja chombo kimoja kinachosafiri majini?
5. Abiria ni nani?

**SEHEMU YA 2: KUSOMA**

**Zoezi la 1: Kusoma kwa sauti.**

Jana jioni mimi na babu yangu tulikuwa tukisikiliza redio. Wimbo niliupenda ulipoisha, matangazo yalianza. Katika matangazo, redio ilitangaza kuwa makali ya ugonjwa wa Korona yalikuwa yamepungua nchini. Habari hiyo ilitufurahisha sana. Tulitakiwa kuendeleza uvaaji wa barakoa na unawaji wa mikono.

**Alama 10**

**Zoezi la 2: Kusoma kwa Ufahamu.**

**Soma hadithi na ujibu maswali yafuatayo.**

Jumapili moja, panya alimtembelea paka aliyekuwa akiishi pangoni pamoja na watoto wake watatu. Panya alipofika pangoni, alibisha hodi mlangoni lakini hakuna aliyemjibu. Baadaye, alimwona paka na kikapu chake kilichojaa matunda. Paka alikuwa ameenda shambani kuvuna matunda. Wote walikaa chini ya mti na kuyafurahia matunda hayo.

11. Panya alimtembelea paka siku ya \_\_\_\_\_.
12. Paka alikuwa akiishi \_\_\_\_\_ pamoja na watoto wake.
13. Je, paka alikuwa na watoto wangapi? \_\_\_\_\_.
14. Paka alibeba kikapu kilichojaa \_\_\_\_\_.
15. Wote walikaa chini ya \_\_\_\_\_ na kuyafurahia matunda.

**SEHEMU YA 3: SARUFI**

**Tumia "hii" au "haya" kwa usahihi.**

16. Maji yaliyochafuliwa na bata ni \_\_\_\_\_.
18. Matunda \_\_\_\_\_ ni ya nani?
19. Kazi niliyofanya ndiyo \_\_\_\_\_.

**Tumia herufi kubwa panapofaa.**

20. leo ni siku ya jumatatu. \_\_\_\_\_.
21. nchi ya kenya ina amani. \_\_\_\_\_.
22. nilimwona anjela uwanjani. \_\_\_\_\_.

**Tumia "vizuri" au "vibaya" kwa usahihi.**

23. Ni \_\_\_\_\_ kuwaheshimu walimu wetu.
24. Mtoto alianguka akaumia \_\_\_\_\_.
25. Chakula kikipikwa \_\_\_\_\_, huwa kitamu.

**SEHEMU YA 4: KUANDIKA**

**Ziandike upya sentensi zifuatazo.**

26. Siku yangu ya kwanza shuleni, niliogopa.  
\_\_\_\_\_
27. Mama yangu aliniacha ofisini.  
\_\_\_\_\_
28. Mwalimu wangu alikuja na kunichukua.  
\_\_\_\_\_
29. Alinikaribisha katika darasa la chekechea.  
\_\_\_\_\_
30. Baadaye nilizoea maisha ya shuleni.  
\_\_\_\_\_